

Kuwa na Uhusiano Mzuri Pamoja na Ndugu au Dada Zangu

“Endeleeni kuvumiliana na kusameheana kwa hiari ikiwa yeyote ana sababu ya kulalamika juu ya mwingine.”—Wakolosai 3:13.

Ni jambo muhimu kujifunza jinsi ya kusuluhisha matatizo, na sehemu nzuri ya kuanza kufanya hivyo ni katika familia. Tumia maswali yaliyo chini kutambua, kuchanganua, na kusuluhisha hali ya kutoelewana kati yako na ndugu au dada yako.



TAMBUA TATIZO

Kati ya ndugu na dada zako ni yupi ambaye unaona ni vigumu kuelewana naye?

Ni jambo gani hasa ambalo huchochea ugomvi kati yenu?

Mara nyingi ugomvi hutokeaje?

Ndugu au dada yangu anapo . . . (eleza jambo analofanya)

nina . . . (eleza jinsi unavyotenda)

na kusababisha . . . (eleza hali inayotokea)



CHANGANUA TATIZO

BIBLIA INASEMA HIVI:
'Endeleeni kuangalia, si faida za kibinafsi za mambo yenu wenyewe tu, bali pia faida za kibinafsi za wengine.' (Wafilipi 2:4)
Ukiwa na jambo hilo akilini, jaribu kuelewa maoni ya ndugu au dada yako.

Ndugu au dada yako alikuwa akifikiria nini alipogombana nawe?

Ikiwa ndugu au dada yako angeulizwa angesema wewe ulichangiaje kutokea kwa ugomvi huo?

Unaweza kupata faida gani ukizingatia maoni ya ndugu au dada yako?



SULUHISHA UGOMVI

Je, mnaweza kujadiliana au kukubaliana? Ikiwa ndivyo, unaweza kufanya hivyo jinsi gani?

Unaweza kufanya nini wakati ujao ili kutoelewana kusitokeze matatizo makubwa?



ORODHA YA KANUNI ZA BIBLIA

Ni kanuni ipi kati ya hizi zilizoordheshwa unayoweza kutumia wakati ujao ugomvi kama huu unapotokea?

- “Pendaneni sana kutoka moyoni.”—1 Petro 1:22.
- “Usawaziko wenu na ujulikane kwa watu wote.”—Wafilipi 4:5.
- “Usiwe na haraka kuudhika katika roho yako, kwa maana kuudhika hukaa katika kifua cha wajinga.”—Mhubiri 7:9.
- “Mwanzo wa ugomvi ni kama mtu anayefungulia maji; kwa hiyo kabla mabishano hayajalipuka, jiondokee.”—Methali 17:14.
- “Pasipo na kuni moto huzimika, na pasipo na mchongezi ugomvi hutulia.”—Methali 26:20.
- “Kwa nini unautazama unyasi ulio katika jicho la ndugu yako, lakini hulifikirii boriti lililo katika jicho lako mwenyewe?”—Mathayo 7:3.

Mwishowe, andika jambo moja ambalo linakufanya umthamini au kumheshimu ndugu au dada yako.

UTAFANYA NINI?

BIBLIA INASEMA HIVI:
“Kuna mtu anayesema bila kufikiri kama kwa upanga unaochoma, lakini ulimi wa mwenye hekima huponya.”
—Methali 12:18.

“Baba alipolazwa hospitalini kwa muda mrefu, ilikuwa vigumu kwangu kumtembelea kwa sababu sikuweza kuendesha gari. Nili-mwomba ndugu yangu mkubwa anifundishe kuendesha gari ili nipate leseni ya kuendesha gari lakini aliniambia ana mambo mengi ya kufanya hivyo hana muda wa kunifundisha. Hata nilipomweleza sababu ya kutaka kujifunza kuendesha gari, alipuuza mambo niliyomweleza. Nili-kasirika sana, na nikamwambia ndugu yangu kuwa hajali hisia zangu kwamba ninahitaji kumwona baba. Jambo hilo lilimumiza. Tulizozana na kila mmoja alieleza jinsi mwenzake alivyokosa kumfikiria.”—**Karina.**

Ikiwa ungekuwa Karina, *ungefanya* nini ili kusuluhisha hali hii?

KILE ALICHOFANYA KARINA: “Siku iliyofuata tulikuwa na mazungumzo mazuri na ndugu yangu. Aliniomba msamaha kwa sababu ya kukasirika na alinielea mambo yote aliyokuwa akikabili. Sikujua kwamba alikuwa na mambo mengi sana aliyohitaji kuyashughulikia. Aliponielea jinsi alivyohisi, nilimwomba msamaha kwa kujaribu kumtwika mzigo zaidi. Ninajua niliomba jambo la maana lakini haukuwa wakati unaofaa wa kufanya hivyo.”

